# DARASA LA SABA MUHULA WA KWANZA 2018

## KISWAHILI

***JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU***

1. *Tumia penseli ya kawaida.*
2. *Hakikisha umeandika kwa karatasi ya majibu:*
   ***(I) JINA LAKO*** ***(II) JINA LA SHULE YAKO***
3. *Kwa kila swali onyesha jibu sahihi kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndiyo jibu.*

---

**Soma vifungu vifuatavyo kisha ujaze nafasi zilizoachwa wazi kwa jibu sahihi.**

Ukimwi ni ugonjwa __1__ na tabia za kujamiana. Jambo hili limekuwa tatizo kubwa katika __2__ nyingi za dunia. Umma unaoishi mahali __3__ hakupatikani maadili na utu huwa __4__ nguvu za kuangamiza __5__ za kuzuilia gonjwa hili. Kwingineko tatizo huwa la kutopata maarifa ya kukinga mwili kutokana na jamba hili. Katika hali namna __6__ suluhisho ni kuelimisha watu __7__ ya kujikinga kwani kinga ni bora kuliko tiba.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. unaosababisha | B. unaosababisha | C. unaosababishwa | D. unaosababishana |
| 2. | A. pembe | B. kuta | C. bahari | D. nyumba |
| 3. | A. ambapo | B. ambamo | C. ambalo | D. ambako |
| 4. | A. hauna | B. hakuna | C. hawana | D. haina |
| 5. | A. ila | B. wala | C. bali | D. ili |
| 6. | A. hizi | B. hili | C. hivi | D. hii |
| 7. | A. mbinu | B. harakati | C. jinsi | D. hatua |

Rafiki __8__ panga ananienzi na __9__ __10__ chanda na pete __11__ wetu ni wa kufa __12__ panga ni mwungwana si kidogo ana umri __13__ miaka __14__ nilimjua na __15__ tangu awali, kwetu na kwao ni karibu kama pua na mdomo.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 8. | A. wangu | B. yangu | C. zangu | D. yetu |
| 9. | A. kunichukia | B. kinitweza | C. kunipenda | D. kunikejeli |
| 10. | A. lau | B. kama | C. ila | D. mithili |
| 11. | A. usuhuba | B. uadui | C. kupenda | D. ushuhuda |
| 12. | A. kupona | B. kuzikana | C. kucheka | D. kulia |
| 13. | A. wa | B. ya | C. za | D. la |
| 14. | A. kumi na tano | B. kumi na mbili | C. kumi na sita | D. kumi na tatu |
| 15. | A. kumfahamu | B. kumwona | C. kumbeza | D. kumjali |

***Kutoka swali la 16-30, chagua jibu sahihi kulingana na maagizo***

**16.** Chagua neno ambalo si kitawe.

A. Mto B. Duma

C. Kima D. Kaa

**17.** ***Chagua kiunganishi sahihi kukamilisha sentensi***

Yeye ni tajiri sana ______ hana watoto wa kumrithi.

A. madhali B. wala

C. aidha D. japo

**18.** Mtoto wa nzige huitwa __________

A. shibli B. kimatu

C. kiweto D. kinegwe

**19.** ***Chagua usemi wa taarifa ufaao wa sentensi***

"Ukila utashiba sana", mama alisema.

A. Mama alisema ungekula utashiba sana

B. Mama alisema kuwa akila atashiba sana

C. Mama alisema kuwa angekula angeshiba sana

D. Mama alisema ukila utashiba sana

**20.** Neema ni mtoto wa dada yangu. Kwa hivyo Neema ni nani?

A. Mpwa wangu

B. Kining'ina changu

C. Binamu yangu

D. Kilembwe wangu

**21.** Tumia kirejeshi: Mgeni ambaye atafika ni mcheshi

A. Mgeni atakayefika ni mcheshi.

B. Mgeni afikaye ni mcheshi.

C. Mgeni atayefika ni mcheshi

D. Mgeni ambaye atakayefika ni mcheshi

**22.** Maafisa, mitume na viroboto ni nomino katika ngeli ya:-

A. I-ZI B. A-WA

C. U-ZI D. I-I

**23.** Malipo kwa mtu aliyeudhiwa ili kumtuliza hasira huitwa ________

A. fidia B. mapoza

C. ridhaa D. dia

**24.** Chagua kivumishi katika sentensi ifuatayo.

Safari ndefu huanza kwa hatua ya kwanza

A. Safari

B. Ndefu

C. Hatua

D. Kwanza

**25.** **9,006,009** kwa maneno ni ________

A. tisa milioni, mia tisa elfu na sita

B. tisa milioni, elfu mia tisa na tisa

C. tisa milioni, laki sita na tisa

D. tisa milioni, sita elfu na tisa

**26.** Machungwa ishirini pamoja huitwa ______ moja ya machungwa.

A. darzeni

B. bunda

C. jozi

D. korija

**27.** Chagua sentensi inayoonyesha "kwa" ya nia.

A. Alitembea kwa madaha

B. Naenda kwa nyanya kulima

C. Alitimua mbio kwa kujisalimisha

D. Alisafiri kwa baiskeli

**28.** ***Kanusha sentensi:***

Wimbo uliimbwa na ukafurahisha

A. Wimbo uliibwa na ukuaudhi

B. Wimbo uliimbwa na haukufurahisha

C. Wimbo haukuimbwa na ukaudhi

D. Wimbo hukuimbwa wala kufurahisha

**29.** ***Tegua kitendawili.***

Hana haja ya kukaribishwa _______

A. nzi

B. jirani

C. mgeni

D. nyoka

**30.** Masalkheri ni sungura ndiko kusema kuwa masalkheri __________

A. pengine ni mjanja

B. yamkini ni mjanja

C. ni mjanja

D. si mjanja

***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31-40.***

Mawingu yalionyesha ishara kuwa mvua ingenyesha wakati wowote. Wakulima walikuwa na bashasha kwa sababu hawakuwa wamepata mvua kwa misimu miwili iliyopita. Mifugo ilikuwa haionekani mahali popote.

Hapakuwa na sababu yoyote ya kufyeka. Moja kwa moja wakulima walianza kulima. Nilikuwa na **maksai** wanne ambao walinisaidia kulima.

Sehemu ile ilikuwa tambarare na kuna wakati maji hutuama. Niliamua kupanda mpunga. Majirani waliangua vicheko kwa sababu mpunga huhitaji maji mengi na ukame ulikuwa umetawala sehemu ile. Watu wengi waliacha kulima mimea na kupanda mikashorina, miti ambayo hustahili joto na ukame. Sehemu ile ilibadilika kuwa msitu wa kutisha uliokuwa na wanyama sampuli zote.

Niliamua **kusia** mbegu kabla mvua haijanyesha. Baada ya siku kumi na nne, mvua ya rasharasha ilianza kunyesha. Ilinyesha **kidindia** kwa siku tano. Mpunga ulichipua vizuri. Waliopanda mbegu za mimea mbalimbali ilichipua vizuri na kuonyesha tumaini kuwa huenda wangepata mavuno mazuri. Mvua ilipusa kwa juma moja na jua likawaka kwelikweli. Ardhi ilianza kukauka tena katika zile hekaheka za kulalamika na wenye imani kumwomba Jalali awajalie mvua, ilianza kunyesha. Si rasharasha tena. Ilikuwa ya masika. Ilinyesha mchana na usiku. Kwa sababu sehemu ile ilikuwa tambarare, maji yalituama. Mpunga ulinawiri vyema lakini mimea mingine ilinyauka na majani yake kuwa manjano. Matumaini yalitoweka tena. Mafuriko yaliwahangaisha wenyeji. Mbu walijaa kama nzi na kila wakati watu walifurika hospitalini wakitafuta matibabu. Utafiti wa maradhi na dawa mujarabu vilisaidia kuepuka mauko yoyote.

Baada ya mafuriko kuisha, nilikuwa na gange kubwa ya kuvuna mpunga. Mavuno yalikuwa mazuri sana. Bei ya mchele ilikuwa imepanda sana. Nilipata faida kubwa. Kuanzia wakati ule, wakati wa mvua ya masika huitwa msimu wa mpunga.

**31.** Kwa nini wakulima walikuwa na bashasha?

A. Mvua ilikuwa ikinyesha kila siku

B. Walitarajia mvua ambayo walikaa muda mrefu bila kuipata

C. Mawingu yalionekana angani

D. Walikuwa na mavuno mengi

**32.** Kulingana na aya ya kwanza mifugo:-

A. walikuwa wamekonda na kukondeana

B. walikuwa hawaoni chanikiwiti

C. walihamia mahali kwenye nyasi

D. walitarajia mvua

**33.** Kwa nini wakulima hawakufyeka?

A. Walichoma nyasi zote

B. Hapakuwa na nyasi zozote

C. Mvua ilikuwa imeleta mafuriko

D. Mvua haikunyesha kwa muda mrefu

**34.** Neno **maksai** kama lilivyotumika ni nini?

A. Fahali waliohasiwa wanaotumiwa kulimia

B. Wafanyakazi wa kibarua waliolipwa kila siku

C. Waajiriwa wa mshahara

D. Wapanzi wa mimea

**35.** Unafikiria ni nini kilichosababisha mvua kunyesha?

A. Maombi ya wakristo

B. Ukame wa muda mrefu

C. Mikashorina iliyopandwa

D. Maajabu ya ulimwengu

**36.** Mvua kunyesha **kidindia** ina maana gani?

A. Mvua ilinyesha mfululizo bila kupusa

B. Mvua inayosababisha mafuriko

C. Mvua ya rasharasha

D. Mvua inayopusa baada ya muda mfupi

**37.** Ni nini maana ya kusia kama lilivyoyumika?

A. Kupanda mpunga shambani

B. Kupanda mbegu bila kuchimba makoongo

C. Kupanda mbegu kabla mvua kuanza

D. Kupanda mbegu baada ya mvua

**38.** Mvua kucha kunyesha ni __________

A. kukoma B. kuzira

C. kupusa D. kupukusa

**39.** Ni ugonjwa gani ambao ungekuwa nadra kuwashika wakazi wa sehemu ile?

A. Kichocho

B. Malaria

C. Kipindupindu

D. Kifaduro

**40.** Ni methali gani ambayo inaweza kufaa katika habari hii?

A. Hakuna masika yasiyokuwa na mbu

B. Kipya kinyemi ingawa kidonda

C. Dawa ya moto ni moto

D. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu

***Soma habari hii kisha ujibu maswali 41-50.***

Uchaguzi wa mwaka wa elfu mbili na saba nchini Fisadi ulikuwa wa kusisimua na vilevile wa kushangaza. Mahuluki walijitokeza kwa wingi katika maeneo bunge yote ili kumchagua kiongozi wao. Kila mja alijikakamua vilivyo na kupiga kura kwa hamu na shauku ghaya. Chambilecho wenyewe, walichoshwa na kuchushwa na katiba iliyokuwa na hitilafu chungu nzima.

Wananchi walichoshwa na ukosefu wa usalama katika mitaa kadhaa wa kadhaa nchini, uhaba wa vyakula na hata siha nzuri. Ajabu ni kwamba baada ya uchaguzi ambao waliona ndiyo kamba ya matumaini, kulibainika waz kwamba kulikuwa na wizi wa kura. Jambo hili lilizua zogo na zahama nchini kwani hakukueleweka aliyekuwa mshind wa kura za Urais.

Pindi tu mshindi alipotangazwa, vita vya kikabila vikazuka katika kila janibu ya nchi. Katika hekaheka hizi, mal ya watu yaliporwa kabisa na mengine kuharibiwa kwa kuteketezwa. Nyumba nyingi vilevile zilitiwa moto na kubaki majivu tu. Watu wengi walihama makwao na kuwa wakimbizi wa ndani kwa ndani katika nchi yao. Aibu iliyoje! Walioishi mipakani wakakimbilia nchi jirani kusalimisha roho zao. Takribani watu elfu moja walipoteza maisha ya na wengine takribani nusu milioni kukosa makao.

Fauka ya hayo, kulikuwa na adha nyingi sana zilizotokea baada ya uchaguzi huo. Watalii wengi ambao walikuw wakizuru nchi yetu walisitisha ziara zao kwani hakukuwa na usalama wa kutosha. Nayo sekta ya biashara pia ikazu balaa kama si beluwa kwa kupandisha bei ya bidhaa muhimu. Aidha nauli ilipanda na kuathiri sana wananchi na hat nchi jirani.

Katika kambi za wakimbizi ya Firauni yalishuhudiwa wakati ambapo maradhi ya zinaa yalisambazwa kw urahisi. Vilevile magonjwa kama kifua kikuu, kipindupindu, taifodi na mengineyo yaliambukizwa.

**41.** Uchaguzi wa mwaka elfu mbili nchini Fisadi ulikuwa wa kusisimua kwa kuwa:-
- A. insi wengi walijitokeza
- B. mahuluki wengi hawakujitokeza
- C. insi wengi walisisimka
- D. ulisisimua na kushangaza

**42.** Kwa nini kila mja alijikakamua kupiga kura kwa ari?
- A. Walichoshwa na kuchushwa
- B. Katiba ilikuwa rasimu
- C. Katiba iliyokuwa ilikuwa na dosari
- D. Katiba ilikuwa chungu nzima

**43.** Wananchi walichoshwa na haya ila:-
- A. mfumuko wa bei ya bidhaa
- B. uhaba wa vyakula
- C. ukosefu wa kazi na afya nzuri
- D. usalama bora katika mitaa kadhaa

**44.** Kisawe cha neno zogo ni:-
- A. ukete
- B. uraufu
- C. tandabelua
- D. utulivu

**45.** Vita vilizuka kila janibu _______
- A. kabla ya mshindi kutangazwa
- B. uchaguzi ulipokuwa ukiendelea
- C. tume ya uchaguzi ilipovunjwa
- D. baada ya mshindi kutangazwa

**46.** Tunasema mali yaliporwa aidha nyumba _______
- A. yaliteketezwa
- B. ziliteketezwa
- C. uliteketezwa
- D. paliteketezwa

**47.** Waliopoteza makao ni takribani _________
- A. watu elfu moja
- B. watu laki moja
- C. watu milioni moja
- D. watu milioni mmoja

**48.** Nchi ya fisadi iliathirika vipi?
- A. Katika sekta ya utalii
- B. Kiuchumi
- C. Katika muundo msingi
- D. Mipakani

**49.** Kamilisha methali. ................................. utaor Firauni.
- A. Ukistaajabu ya Firauni
- B. Ukistaajabu ya Musa
- C. Ukistaajabia ya Musa
- D. Ukistaajabika ya Firauni

**50.** Ni mada ipi itafaa kwa habari hii?
- A. Mjenga nchi ni mwananchi
- B. Amani haiji ila kwa ncha ya upanga
- C. Alla Alla jirani kama ndugu mli kule
- D. Dunia mtego wa panya